JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Bodi ya Usajili wa Wathamini

**Chuo Kikuu cha Dodoma, shule ya CIVE**
**Jengo la Utawala, Ghorofa ya 1,**
**S. L. P. 325, Dodoma, Tanzania**
**Simu Na: +255 733542654, Barua pepe: registrar@vrb.go.tz**

# TANGAZO KWA WATHAMINI WOTE NCHINI

## MALIPO YA ADA ZA USAJILI, LESENI NA MADENI KATIKA BODI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Wathamini wote nchini katika makundi yao ya usajili na Makampuni ya Uthamini wanakumbushwa kulipa ada za usajili, leseni kwa mwaka 2024/2025 na madeni yao kabla ya tarehe 30 Julai, 2024. Ifikapo tarehe 31 Julai, 2024, Bodi itatangaza kwenye gazeti daftari la Usajili lenye orodha ya Wathamini na Makampuni ya uthamini wanaoruhusiwa kufanya kazi za uthamini kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Wathamini wote ambao hawatakuwa wamekamilisha malipo yao hawatatangazwa gazetini hivyo hawataruhusiwa kufanya kazi zozote za uthamini. Ni kosa kufanya kazi za uthamini nchini bila ya usajili na leseni kutoka Bodi, kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 25 cha Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini nchini. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa watakaovunja sheria hii kama ilivyoainishwa katika Vifungu namba 43 na 44 vya Sura 138 ya 2016.

Malipo yote yatafanyika kupitia Ofisi ya Msajili kwa kutumia namba za malipo (control number). Kupata namba ya malipo au kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa: barua pepe registrar@vrb.go.tz, na namba za simu: 0733 542654, 0679 521126, 0654 103361.

**MSAJILI**
**02/07/2024.**